




Hali ya malaria katika eneo linaloandaliwa kwa ajili ya utafiti wa chanjo ya malaria wilayani Korogwe

BP Mmbando, DRS Ishengoma, MD Segeja, HA Msangeni, SH Sembuche, MD Seth, EK Malecela, R Madebe, AS Rutta, ML Kamugisha na MM Lemnge

Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu, Kituo cha Utafiti cha Tanga, S.L.P 5004 Tanga, Tanzania

Utangulizi

Mradi wa NIMR-AMANET unafanyika katika vijiji 12 vya wilaya ya Korogwe nchini Tanzania. Mradi unaandaa eneo kwa ajili ya majaribio ya chanjo ya malaria. Baadhi ya vijiji hivi vipo katika maeneo ya miinuko na vingine katika mabonde. Vijiji vya mabondeni vinajumuisha vijiji vilivyoko jirani na mji wa Korogwe na vijiji vilivyoko mbali na mji. Maambukizi ya ugonjwa wa malaria yanatofautiana katika vijiji hivi na kwa ujumla ni madogo kwenye maeneo ya miinuko. Hali ya maambukizi ya malaria ni ndogo katika maeneo ya mjini ukilinganisha na vijijini kwa sababu ya ubora wa maisha uliopo mijini.



Utaratibu

Tafiti nne zilifanyika katika vijiji 12 wakati wa mvua za vuli na masika kuanzia Novemba 2005. Dodoso kuhusu ugonjwa wa malaria zilijazwa kwa wale wote waliokubali kwa hiari (au wazazi/walezi wao) na wenye umri kati ya miaka 0 -19. Vimelea vya malaria vilichunguzwa, upungufu wa damu na ukubwa wa bandama ulipimwa. Sampuli za damu zilichukuliwa kwa ajili ya vipimo vya kinga na vipimo vingine katika maabara hapa nchini na nje ya nchi. Vijiji vinne kati ya 12 vilihusishwa katika upimaji wa homa na vimelea vya malaria kwa kutumia wahudumu wa afya ya msingi vijijini ambapo wagonjwa wote wasio na malaria kali walitibiwa kwa kutumia dawa zilizopendekezwa na Wizara ya Afya.

Matokeo

Jumla ya watu 10,971 walipimwa katika hizo tafiti nne. Maambukizi ya vimelea vya malaria yalikuwa makubwa katika vijiji vilivyoko katika maeneo ya mabondeni, mbali ya miji. Hali ya maambukizi katika vijiji vya mabondeni vilivyo karibu haikutofautiana sana na ile ya maeneo ya miinuko (Umbo Na. 1). Watoto wa umri wa miaka 0-5 ndio walikuwa na vimelea wengi wa malaria katika damu kwa sababu ya upungufu wa kinga. Matumizi ya vyandarua yalikuwa makubwa katika vijiji vya mabondeni karibu na miji ambapo asilimia 62 walikuwa wanatumia vyandaru na madogo katika maeneo ya miinuko ambapo waliokuwa wanatumia ni asilimia 38.4 tu. Matumizi ya vyandarua katika watoto chini ya umri wa miaka mitano yalikuwa kati ya asilimia 64.0 na 71 katika vijiji vilivyo karibu na miji ambayo iliwiwiana kabisa na kupungua ugonjwa wa malaria katika maeneo hayo.

Wastani wa kiwango cha damu haukuonesha tofauti sana katika hizo sehemu tatu ingawa watu waliokuwa wanatumia chandarua walionekana kuwa na kiwango cha juu cha damu. Watu walikuwa na vimelea vya malaria walionekana kuwa na upungufu wa damu. Upungufu wa damu ulionekana zaidi katika maeneo ya mabondeni yaliyoko mbali na mji.

Hitimisho

Utafiti huu unaonesha kuwa hali ya maambukizi ya vimelea vya malaria ni ndogo katika vijiji vya mabondeni vilivyo karibu na mji wa Korogwe. Hii inaweza kusababishwa na hali nzuri ya kijamii na kiuchumi na/au matumizi makubwa ya vyandarua. Eneo hili la utafiti kwa sasa limefikia viwango vinavyotakiwa na litashiriki katika tafiti za chanjo ya malaria. Kutokana na takwimu za utafiti huu na ule wa CORPs na DSS, kijiji cha Kwashemshi kilichaguliwa kushiriki katika awamu ya kwanza ya chanjo ya malaria iitwayo MSP3 chini ya ufadhili wa AMANET.

Shukrani: Tunapenda kuwashukuru viongozi na wanakijiji wote kwa kushiriki katika utafiti huu. Tunawashukuru sana wataalamu wote waliofanikisha kazi hii; F Francis, J Akida, M Chille, J Sadi, M Munisi, Z Maumba, H Athumani and J Tupa. Pia tunawashukuru madereva wetu ndugu Z Kauzeni na T Semdoe. Mradi huu ulifadhiliwa na shirika lisilo la kiserikali liljulikanalo kama African Malaria Network trust (AMANET) **Kwa maelezo zaidi wasiliana na: Dr. Martha Lemnge, S.L.P. 5004, Tanga, E-mail: mlemnge@tanga.mimcom.net**